*Jiwe la Kiroho la Kujengea na 11.*

# KWA ROHO YA UPOLE MPOKEE CHRISTO, NENO.

***Yakobo 1:19-21*** *"Hayo mnajuwa , ndugu zangu wapenzi basi kila mtu na awe mwepesi wa kusia, bali si mwepesi wa kusema, wala kukasirika kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu kwahiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lilopandwa ndani liwezalo kuliosha roho zenu".*

Kitu cha pekee kischo na hatia tulicho nacho, nawazia, itakuwa ni kondoo, Mungu alipotaka kumtambulisha Yesu Kristo alimtambulisha Yeye kama mwana Kondoo ***(Mathayo 3 :13-17).*** Na alipotaka kujitambulisha yeye mwenyewe alijitambulisha mwenyewe kama ndege, hua na aliye msafi kuliko ndege wote waishio, na mwana Kondoo ndiye pekee asiye na hatia na msafi kati ya mwana waishio, na mwana kondoo ndiye pekee asiye na hatia na msafi kati ya wanyama wasihio.

Yesu alibatizwa na Yohana na Bibilia ilisema, "Nae aliona Roho wa Mungu, akishuka kama hua, akija juu yake" ***(Yohana 1:29-34)*** kwa iyo kama angekuwa ni mbwa mwitu, au kama angekuwa mnyama mwingine yeyote ile asili ya huwa isingeweza kukubaliana na ile asili ya mbwa mwitu, kadhalika asili ya hua isingeweka kuungana na mnyama mwingine yeyote isipokuwa kondoo, Sasa hzi asili mbili zilikuja pamoja, hapo sasa zilikubaliana moja kwa nyingine.

Sasa unaona kule kuchaguliwa kimbele ilikuwa ni mwana Kondoo alipo kuja pale alizaliwa akiwa Kondoo alilelewa akiwa kondoo na kwahiyo, hiyo ndiyo aina pekee ya Roho halisi ambayo ingeweza kupokea neno, ambayo ingeweza kupokea Kristo walio bakia wote watajaribu kuipata hiyo, na ukimweka Roho wa Mungu katika mbwa mwitu, unaona yenye hasira isiyofaa, ya kichoyo hataweza kukaa pale. Roho Mtakatifu ataruka mbali mara moja haitawezekana kufanya hivyo ni vipi kama yule njiwa angekuja chini badala ya yeye kuwa kondoo angekuwa mnyama aina nyingine haraka sana angeruka na kurudi zake unaona lakini alipoona asili ambayo anaweza akaungana n ayo ndani, iliweza kuwa kitu kimoja.

Apo, sasa huwa alimwongoza kondoo na angalia alimwongoza kondoo kwenye machinjio ***(Isaya 53:7)*** sasa mwana kondoo alikuwa mtiifu kwa kuwa
***(Wafilipi 2:5-11)*** haijalishi alimwongoza wapi alikuwa tayari kwenda nashangaa leo kama Mungu angejaribu kutongoongoza maisha yetu kuweza kujisalimisha kabisa na kuweza kumtumikia yeye (***Warumi 8:36-37)*** nashangaa kama Roho zetu wakati mwingine zinahasi zikijaribu kuonyesha kwamba, sisi ni kondoo mwana kondoo ni mtiifu.

Kondoo anaweza kujitoa kuwa sadaka haina madai yake mwenyewe anaweza akaa haina madai yake mwenyewe anaweza akalala chini nawe umnyowe manyoya yake yote na icho ndicho kitu alichonacho. Kamwe asemi chochote juu ya hilo anatoa sadaka kila kitu alichonacho huyo ni kondoo anatoa vitu vyote vichukuliwe yenyewe na vyote alivyonavyo na hivyo ndivyo hasa Mkristo halisi alivyo anajitolea sadaka wenyewe bila kujali chochote cha mambo ya ulimwengu wakujitolea sadaka wenyewe bila kujali chochote cha mambo ya Ulimwengu wa kujitolea vyote walivyonavyo kwa Mungu. [1]

Kondoo ni mpole sana kiasi kwamba anaweza akiongozwa na iyo ndiyo sababu Mungu alimwakilisha Kristo kama Kondoo na yeye mwenyewe kama huwa na siku ile Yohana alipombatiza Yesu pale mtoni ya undani moja ya matukio makuu sana yaliwahi kutokea yalitokea pale angalia ilivyo nzuri kondoo akiwa mpole kuliko ndege wote wa angani sasa hiyo ndiyo njia pekee ingeweza waungane.

Njia ya pekee ambayo ingemfanya kuja juu ya Kondoo sasa wakati huwa aliposhuka chini Yohana alimwona Yesu naye akasema “tazama mwana kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi za Ulimwengu” ***(Yohana1:29-33)*** na Yohana akasema ninashuhudia kumwona Roho wa Mungu akishuka kama huwa na kukaa juu yake haleluya upo hapo Yule huwa na kukaa juu yako haleluya upo hapo Yule huwa mwana Kondoo waliungana pamoja apo ndipo Mungu na mwanadamu walipokuwa mmoja hapo ndipo mbingu na dunia zilipo kumbatiana pamoja haleluya hapo ndipo Mungu alipofanyika mwili ilitokea hapo ***(Timotheo 1:3:16)*** hapo ndipo Mungu aliposhuka chini kutoka kwenye umbo la Roho na kufanyika mwanadamu naye kukaa pamoja nasi ndipo milele yote ilipokumbatiana pamoja nasi ndipo milele yote ilipokumbatiana pamoja hapo ndipo mwanadamu walio anguka uzao wa adamu na Jehova Mungu na kila malaika alipokuja pamoja. Wakati Mungu na binadamu alipofanyika mmoja katika siku ile kuu ya kumbukumbu wakati Yohana alipo mbatiza Yesu sasa vipi kama ingekuwa mbwa mwitu [2]

Siku ile Yohana alipombatiza Yesu kondoo Yohana alisema “apo unakuja upole wa Mungu tazama kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya Ulimwengu
***(Yohana 1:29)*** na wakati Yohana alipo mbatiza yeye nay eye akatoka kwenye maji, Roho Mtakatifu katika umbo la huwa alishukan juu yake na kukaa ndani yake Amina akakaa ndani.

Hilo lilikuwa ni tukio kuu mno ambayo dunia iliwai kuona na itakuja kuona mpaka Kristo na Kanisa watakapo ungana tena, hapo ndipo Mungu na mwanadamu watakapo ungana tena, hapo ndipo Mungu na mwanadamu watakapo watakapo kuwa mbingu na dunia inakumbatiana pamoja na kusiana pamoja na kumaliza swala la dhambi milele ***(2Klokorintho 5:17-19)*** hapo ndipo huwa na kondoo imeungana pamoja hapo ndipo ule patanisho mkuu uliwahi kufanyika ni pale Mungu wa kristo walipounganinika na kuwa pamoja na marafiki ngoja niwaambie kitu fulani sisi ni kondoo wa munguemetulinganisha na kondoo zake
***(Yohana 10:1-30)*** [3]

Yohana alimuona mtu mmoja kijana akimjia akaona ile nguzo ya moto katika umbo la hua ikishuka chini kutoka mbinguni na sauti ilisema “huyu ni mwanangu mpendwa anaye pendezwa kupoa ndani yake” yohana alisema “ ninashuhudia kwamba yeye aliniambia kule jangwani sio kule seminari ni kule jangwani alisema Yule atakaye muona Roho anashuka na kukaa juu yake Amina huyo ndiye atakaye batiza kwa Roho mtakatifu na kwa moto ***( Yohana 1:33)***

Nami nashuhudia kwamba ni kweli ***(Mathayo 3:11-12)*** huyu Mesia alikua ni nani Mesia alikua neno katika ukamilifu wake wote alikua ni ukamilifu wa Mungu ***( kolosai 2:9-10)*** manabii walikua ni nuru kidogo inayoangaza lakini ndani yake ilikua ni nuru yote ilikua ndani ya huyu masihi kwa sababu alikua udhihilisho wa Mungu aliyefanyika Imanuel Mungu pamoja nasi katika mwili wa kibinadamu ***( mathayo 1:22-23)*** [4]

Yule baba akua amekaa ndani yake wakati huo kwa sababu alikuja siku aliopo batizwa yeye [5]

Tukizungumza kiroho wakati Roho alipokuja juu yake siku akibatizwa Yohana akawa masihi mpakwa mafuta …………………sasa kumbuka yeye alikua ni mwana wa Mungu wakati alipo zaliwa alikua ni mwana wa mungu aliyezaliwa kibikira ***( Yohana 1:16-18)*** , ***( Isaya 1:14)*** Luka alipo fanyika masili ni pale Roho mtakatifu alipokuja juu yake kwa sababu masihi maana yake ni yule mpakwa mafuta alikua ni mpakwa mafuta Roho mtakatifu alipokuja juu yake
***(Yohana 1:40-42)*** [6]

Ni kawaza jinsi Mungu na hua ni ndege anayependa sana Mungu akitaka kufanya mapenzi na watu wake Mungu anataka kupendwa alafu Mungu anataka kupenda wewe " Mungu aliupenda sana ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa peke ili kila mtu amwaminie yeye asipotee bali awe na uzima wa milele" ***(Yohana 3:16)***
Bwana abarikiwe hapo Mungu anapenda kufanya mapenzi ilibidi afanye kitu kinapendeka ilibidi atengeneze kitu kipole kama yeye mwenyewe ilibidi atengeneze kitu ambacho ni sawa na na akili yake uwezi ukapenda kitu ambacho sio asili yake mwenyewe kupenda inabidi iunganike na upendo mwanaume na mwanamke inabidi wapendane mmoja kwa mwingine kama itabidi wastahili familia inabidi ipendane mmoja kwa mwingine kama wa tastahili chunguza kila kitu tafuta mwanamke mdogo ambaye atakua mkeo ambaye unampenda naye anatafuta mwanaume ambaye anaweza kumpenda na Mungu anatahita akijaribu kutafuta nafsi ambayo anaweza kuipenda kwa hiyo akajilinganisha mwenyewe apa duniani kama hua mpole na kama kondoo mpole
Jinsi alivyokuwa mpole siku zote hakujaribu kufanya yeye mwenyewe hakujaribu kujifanya anayejitosheleza alisema sifanyi chochote mpaka kile baba anachonionyesha Mimi na baba anakaandani yangu ***(Yohana5:19)***

Sasa jambo jingine kondoo alivyo, kondoo yuko tayari kuachia haki zake.Mungu anatutaka sisi tuwe kondoo, lakini mara nyingi sana hatutaki kuachia haki zetu. Wengi wenu mnasema, "vema ninayo haki ndugu Branham" Hiyo ni kweli lakini je uko tayari kusamehe/kuachlia haki yako? Uko tayari kuachilia haki yako ili Mungu akuongoze? Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu yaliyo mengi leo.
Sisi tunapaswa kuwa kondoo, tumekuwa vitu vyote isipokuwa wanakondoo.Na hiyo ndiyo sababu mara tu, tupatapo huo mtazamo, Yule hua na Roho mtakatifu anaruka na kuondoka kama yule kondoo wa Mungu angefanya huo mng'ako mmoja kama mbwa mwitu, au angefanya chochote kinyume na hua mpole kile angevumilia,yule hua angeruka kwenda zake. Angeondoka mara moja.

Na hiyo ndiyo sababu tunashangaa, kuna tatizo gani na kanisa la kipentekoste. Ni kwasababu tumechukua asili tofauti. Tumechukua asili ambayo, tunataka haki yetu. Tunaenda kufanya kile tunachojua ni sahihi kufanya. Tunakuwa jeuri. Tunajenga uadui, tunakua wasiojali. Tunaruhusu hasira ije. Tunaruhusu ubinafsi uje ukae . Kondoo anamiliki manyoya(sufu)yake,hiyo ni haki yake, wanamchukua kondoo na kumrusha kwenye meza, na kumfunga miguu yake. Kamwe hapigi mateke, kamwe hazozi, unachukua tu haki zake mbali naye, kwasababu yeye ni kondoo. Hawezi kufanya vinginevyo. Kwasababu hiyo ni asili yake .sasa wakati mmoja nenda kinyume na njia ya mkristo, utajua ni kondoo au ni mbuzi.

Utamtambua kile alicho jaribu kwenda kinyume mara moja. Hiyo ndio sababu makanisa yetu yana hali waliyonayo leo.

Huna hali yoyote umenunuliwa kwa gharama hiyo ilikuwa ni bei ya damu ya thamani ya mwana wa Mungu. ***(1 petro 1:17-21)*** huna hali za kisheria. Haleluya. Haki pekee ya kisheria uliyo nayo ni njoo katika chemchem iliyojazwa na damu iliyotoka katika mishipa ya Immanuel . Wakati wakosaji wakioga ndani yake husafiwa dhambi za hatia zao. Ndiyo bwana hiyo ndiyo haki pekee uliyo nayo, ni kujisajilimisha mwenyewe katika mapenzi ya Mungu, na hapo sasa Mungu anakuongoza wewe suku zote na kuendelea. ***(Zaburi 78:14)***

Hiyo ndiyo iliyosababisha mambo mengi mageni. Roho Mtakatifu anasema hiyo siyo sahihi. Simamisha mkutano , nenda mbele ninasimamisha pia. Ndugu endelea mbele. Hiyo ni sawa kwa sababu inabidi uongozwe na Roho wa Mungu. Na njia pekee ya kuongozwa na Roho wa Mungu ni kuwa mpole siyo kujua kila kitu ***(Zaburi 25:8-9)***

Oh unafikiri " Ninajua mengi. Unaicha bongo yako inaamshwa nia mpaka haiwezi kufanya kazi yenyewe. Unajua vitabu vyote, na majibu yote , na kigiriki chote na kibrania hiyo ni kweli. Lakini unajua kila kitu hapo sasa hua hawezi kuongoza kwa sababu unajuwa mengu ***(Mhubiri 3:5-8)***

Kondoo hadai kujua chochote. Lazima apate mtu fulani wa kumuongoza yeye. Utukufu. Hilo ndilo hajui chochote Amen! Jambo moja nijuacho ni kuwa Yesu Kristo alikufa kunikomboa mimi [2]

Jinsi lilivyo zuri kuelezewa hapo Yesu ni kondoo na Mungu akiwa huwa na ya kuwa hua asingetua kwa mbwa asili yake siyo sawa. Ilibidi iwe kwa kondoo asili zao mbili inabidi ziwe sawa. Na hiyo ndiyo namna tunavyopaswa kuwa. Asili yetu inabidi ibadilike kutoka mwenye dhambi angurumaye na kuwa kondoo mpole.

Je uliona Yule Hua alimwongoza Kondoo? Na angalia Kondoo alisimamisha vyote alivyokuwa navyo kwa kuwa na angalia hua akimwongoza, kwenda kusubiliwa kwa ajili ya dhambi zetu sisi sote ***(2 Kor 5:2) (Kolosai 1:19-20).***

Sasa Mungu alipotaka kumwakilisha mwanae alimwakilisha kwa myama aliyekuwa msafi sana na mpole alikuwapo duniani. Mnyama aliyekuwa ni Duniani na Mungu alipotaka kujiwakilisha mwenywe katika mbingu alijilinganisha na ndege msafi sana na mpole katika mbingu yule hua.

Sasa hua ni ndege aliyeumbwa kiajabu kwa sababu  ya tabia zake hawezi kula kitu chochote ambacho ni kichafu hawezi kabisa kwa sababu hakuubwa hivyo .

Sasa nimezungumza kuhusu kua akiwa ni kielelezo cha Mungu na kunguru akiwa kielelezo cha mnafiki kunguru anaweza kula ngano. Pamoja na hua lakini huwa anaweza kula ngano, hawezi kula mzoga uliokufa , unaona? hawezi tu kufanya hivyo. Hawezi kuweka hilo tumboni mwake. Wote ni ndege , wote wanakula lakini ni kwanini? Ni ile namna walivyoumbwa.

Na hivyo ndivyo ilivyo na Mkristo halisi. Mkristo tu wa kidhehebu anaweza kuchukua chochote kile lakini Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili hawezi kuchukuwa mambo ya ulimwengu. Ameumbwa tofauti (2 Kor 5:17)

Uchungu unapishana na hicho. Lakini upendo siku zote hukupokea hicho, lile neno la Mungu.  Sasa yeye hana nyongo. Ni kinyume cha yeye. Lakii hakuna hatari kwa sababu hataenda kukila kwani hana hamu na hicho. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa mkristo wa  kweli. Je ulijua ya kuwa  Mkristo wa kweli hana hata dhambi zinazohesabiwa kwake? David amesema “ amebarikiwa mtu Yule ambaye Mungu hamhesabii dhambi”  ***( Zaburi 32:1-2)*** Unapokuwa umeoshwa katika damu ya mwana Kondoo siyo kwa imani ya kuifanya, lakini kwa damu halisi ya mwanakondoo Mungu hakuhesabii chochote ambacho unakifanya. (Warumi  5:9; ***(Rumi 3 :23-26)*** Kwa sababu uko chini ya damu na halioni hilo. ***(Warumi 4:6-8)*** iko damu. Hiyo pekee awezayo kukuona humo hiyo ndiyo namna alivyokuona wewe kabla ya kuweka misingi ya dunia wakati alipo weka jina lako katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo ***(Ufunuo 13:8)*** hapo ndipo anapoweza kukuangalia wewe kwa sababu umekombolewa kutoka katika kila kitu ambacho ulichowahi kufika umeoshwa kwa damu ya kondoo kwa hiyo  hakuna nyongo ndani yako hakuna mazoea ndani jioni yako, kwa sababu damu ya kondoo imefanya hivyo na Mungu hawezi akakuesabia dhambi wewe kwakuwa unalo toleo la dhambi lililokaa pale likikusubiri wewe.

Unasema hiyo inanipa nafasi ya kutosha ndugu brahnam naweza kufanya chochote nitakacho. Mimi siku zote ninafanya siku zote. Lakini mtu kama ataona hasa kile ambacho Kristo  alimtolea Yeye na kugeuka tena na kufanya kitu kinyume na yeye inaonyesha kamwe hajampokea kristo [7] katika ***(Ufunuo 5:5-6)”*** na mmoja wapo wa wale wazee akanambia usilie tazama samba aliye  kabila wa Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu; na zile muhuri zake sababu nikaona katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne na katikati ya wale wazee mwana kondoo amesimama…” Mwana kondoo kwa nini hajamuona huyu mwana kondoo kabla yule alikuwa anakaa katika kiti cha enzi cha baba ndani ya

walinzi Yohana asingeweza kuona ndani pale. Aliweza kuona wale wenye uhai wanne wakiwa wamesimama pale au hawa makerubi wanne wakilinda pale mahali patakatifu aliweza kuona hawa lakini hawakuweza kuona zaidi ya hapa na pale ndani mara moja kulikuwepo na mmoja mwanakondoo. Sasa kuonyesha kwamba hauwa mwana kondoo mnyama kwa sababu alichukuwa kile kitabu kwa yeye aliyekuwa ameketi katika kile kiti cha enzi ***(Ufunuo 5:5-7)*** mwana kondoo alikuwa ni Kristo kwa maneno mengine tabia zake alikuwa ni mpole na mnyenyekevu kama mwana kondoo sasa angalia alikuwa ni mwana kondoo mkombozi kama yule wa kwanza Mungu habadiliki kamwe! Amen! Mkombozi wa kwanza alikuwa ni mwana kondoo wa Mungu aliyetolewa ***(Mwanzo 3:21)*** na hapa tu namwona tena akiwa amefika huku kwenye ufunuo ni mwana kondoo tena kumkomboa nini? Kumkomboa kutoka kwenye hali ya anguko na kutoka kwenye uridhi ulioanguka wa watu waluioanguka mwana Kondoo anakuja tena kumkomboa sisi kukomboa nini anaenda kutukomboa sisi kutokana na nini kitu chochote ambacho kinaenda kukombolewa ni kitu ambacho kilipotea ni kitu Fulani ambacho kilikuwa kimepotea na sasa kinaenda kurudishwa tena anaturudisha tena sisi huyu mwana kondoo anaturudisha sisi wapi vitu vyote tena vilivyo kuwa navyo mwanzoni uzima wa milele tulikuwa warithi wa dunia kamwe hatukupaswa kuwa wagonjwa kamwe hatukupaswa kuwa wazee kamwe hatukuwa na kitu chochote cha kutuchosha hatukuwa na kitu chochote cha kutuchosha hakukuwa na mazishi (msiba) hakukuwa na makaburi hakukua na uovu hakukua na mauti hakukua na nywele nyeupe mabega yaliyo panda hakukua na maombolezo wala kilio tulikua na uzima wa milele tulikua na haki mamlaka katika dunia yote tulikua na Miungu wadogo hapa duniani kulitembelea hapa na pale na kama mti fulani haukua sahihi kusimama mahali fulani tungesema " ung'oko hapa na ukakae pale" na ungefanya hivyo upepo ungekua unavunja na tungekua hatutaki uvume "Nyamazeni na mkatulie na ungefanya hivyo alikuja kufanya nini? Alitukomboa sisi na kuturudisha hayo tena kuturudishia hayo yote tena na sasa ile asili yenyewe inaugua ikisubiri udhihirisho wa mwana wa Mungu kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu. [8].

Kama kwenye kitabu hapa na pale tulipokua tunazunguzia juu ya vitabu viwili kwamba ni kimoja Kitabu cha uzima kitabu cha kwanza cha uzima kinakuja pale ni pale ulipozaliwa katika uzazi wako wa asili Lakini wakati mmoja kule nyuma chini pale kulikuwa na mbegu ndogo ya uhai ikiwa imelala pale ilikufanya ushangae "Ilitoka wapi nini haya mambo ya ajabu" nilikua nasema hivi ni kujichukua mimi mwenyewe kama ambavyo wewe ungeweza kusema " Willium Brahnam alikua mtu mbaya sana" Unaona ni kwa sababu nimezaliwa na Charles na Ela Brahnam katika asili yao mimi nilikua ni mwenye dhambi nimekuja duniani nikiwa mwongo na tabia zote za dunia zilikuwa ndani yangu lakini kule chini ndani kule kulikua na

asili nyingine iliyo kuwepo iliyo chaguliwa Kimbele iliyowekwa pale na Mungu katika mwili huhu kulikua na asili mbili pale. [9]

Na ili mradi huko katikan haya maisha utakua na sehemu usiyo ipenda ya Kimwili ambayo itakusumbua wewe mda wote unaoishi lakini ndani yako umezaliwa upya ***(1 Petrol 1 :23)*** sasa unapoenda kufufuliwa utakua unafanana na Kristo na dhambi zote zinaondoka kutoka kwako unaona hiyo ndilo lenyewe hii ni Roho inayokufa katika mwili unaokufa lakini sasa huwezi ukawa katika miili miwili kwa wakati mmoja lakini unavyoweza ukawa na asili mbili kwa wakati mmoja unapo zaliwa mara ya pili huzaliwi katika namna ya kimwili kama mtoto anapozaliwa lakini kunatokea nini kule kuzaliwa kwa kiroho kunapo kuwa moyoni mwako ambako ni kwa Mungu kuna mwili wa Kiroho unaokuwa kupokea Roho hiyo na unai unapoondoka katika huu mwili unapoletwa hapa duniani na Roho inaingia ndani na Roho inapoondoka kwenye mwili kuna mwili inaongojea "kwa maana tunajua ya kuwa vyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa tunalo jingo litokalo kwa Mungu ***(2 Wakorintho 5:7)*** Unaona hilo ndilo mwili wa kiroho wa watu . [10]

Ninaomba kwamba utamsaidia Mchungaji wetu mpendwa ndugu Nevil umfanye Bwana kuwa aliyejaa neema aliyejaa nguvu na uelewa kwamba atachukua chakula kilicho hifadhiwa na kuwalisha Kondoo wa Mungu ***(Yohana 21:15-17)*** Bwana naomba kuwa hutayaweka magonjwa mbali nasi na ikitokea kwamba tumekuwa wagonjwa kwamba wakumbuke uwepo wa Mungu atoshae damu ya Bwana Yesu ikiwa madhabahuni kufanya upatanisho na ninaomba waweze kuponywa mara moja na ninaomba utaweka mbali na nguvu za shetani kujaribu kuwavunja moyo au kujaribu kufanya vikundi au……waweke tu mbali na nguvu za adui bwana tutakase kwenye neno lako. ***(Waebrania 13:12)*** Jahalia hilo Bwana. [11].

***<u>Nukuu za Kingereza.</u>***

*[1] Ile Ishara (63-0901M) aya 58-66*
*[2] Kanisa na hali yake 956-0805) aya 33,36-44,97-99*
*[3] Mungu akifanya ahadi zake (56-1209A) aya 40-41*
*[4] Ile sauti ya ile Ishara (64-0313) aya 99-102*
*[5] Kitendawili (64-0206B) aya 282*
*[6] Kumiliki malango ya adui (59-1108) aya 79*
*[7] Katika Mbawa za hua mweupe kama theruji (65-1128E) aya 40-51*
*[8] Ufunuo 5 sehemu 2 (61-0618) aya 88-94*
*[9] Shirika (65-1212) aya 44-45*
[10] Maswali na majibu (64-0830E) aya 31,58
[11] Ule muhuri wa saba (6309324E) aya 370.

---

Jiwe la kiroho la kujengea No 11 mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax(+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*